**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**721** **KISWAHILI**

**Time: 3 Hours** **Mwaka: 2023**

---

**Instructions.**

1. Karatasi hii ina Sehemu A na Sehemu B zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali yote kutoka Sehemu **A** na maswali manne (4) kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40**) na Sehemu B ina **alama sitini (60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha majibu.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org
***Prepared by Maria Marco for TETEA***

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii. Kila swali lina alama **Nne (4)**

1. Bainisha neno linalosababisha utata katika sentensi, kisha onesha maana mbili za sentensi hizo ambazo ni:
   (a) Bei ya paa ni shilingi elfu kumi
   **Utata: Paa**
   **Maana:** ***(i) kifaa kinachotumika kuezeka nyumba***
   ***(ii) mnyama wa porini.***

   (b) Alimuandikia barua kaka yake.
   **Utata: Alimuandikia**
   **Maana:** ***i) aliandika barua kwa niaba ya kaka yake***
   ***(ii) aliandika barua ili aitume kwa kaka yake.***

2. Eleza kwa ufupi hatua nne utakazozingatia iwapo utatumia redio kama mbinu ya kufundishia somo la Ufahamu wa Kusikiliza.

   **a. Kuwaandaa wanafunzi katika mazingira tulivu ili waweze kusikiliza kwa makini,**
   **b. kufafanua mambo mbalimbali yanayowatatiza wanafunzi wakati wa kipindi,**
   **c. kuhakikisha na kusimamia wanafunzi wanatekeleza maelekezo (au amri) kutoka kwa msemaji wa redioni,**
   **d. kuwaongoza wanafunzi kufanya marejeo kuhusu maudhui yaliyowasilishwa kwa kuuliza maswali yatakayotokana na habari waliyosikiliza**

3. Tumia hoja nne kufafanua sababu zinazoifanya fasihi kuchukuliwa kama kioo cha jamii.
   **a) fasihi ina kazi ya kuikosoa jamii pale inapokwenda kinyume na matakwa ya jamii**
   **b) kuielimisha jamii yale ambayo hawayafahamu**
   **c) kuiongoza jamii pale inapokwenda kinyume na taratibu zilizokubaliwa**
   **d) kuonesha aina zote za udhalimu, na kutabiri mambo mabaya yanayoweza yakajitokeza katika jamii.**

4. Elezea namna kitabu cha ziada cha somo la Kiswahili kitakavyokusaidia kufundisha somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha pili.
   **a. kitamsaidia kupata maarifa mapana zaidi nje ya yale yaliyopo kwenye kitabu cha kiada**
   **b. kusaidia kupata mazoezi na maswali mbalimbali ya kupimia uelewa wa wanafunzi**
   **c. kupata maudhui ya ziada ambayo hayakufafanuliwa kwenye kitabu cha kiada**
   **d. kutumika kama kitabu cha rejea wakati wa kuandika azimio la kazi na andalio la somo la mwalimu.**

5. Tumia hoja mbili za Kisayansi kukubaliana na kauli inayosema kuwa *Asili ya lugha ya Kiswahili ni Kibantu* kisha toa mfano kwa kila hoja.

   **(a) kufanana kwa msamiati baina ya lugha ya Kiswahili na zile za Kibantu. Kwa mfano, Kiswahili- mtu; Kiyao – mundu; na Kihehe – munu**


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org
***Prepared by Maria Marco for TETEA***

**(b) kufanana kwa maumbo ya maneno yaliyopo kati ya lugha ya Kiswahili na zile za Kibantu.**

**kwa mfano, Kiswahili - ana-chez-a; Kipare - a- vin-a; na Kihehe -i- kin-a,**

**(c) Kufanana kwa miundo ya tungo kati ya zile za lugha ya Kiswahili na zile za lugha nyingine za Kibantu. Kwa mfano:**

**Kiswahili: Mtoto anaimba vizuri.**
**N T E**

**Kihehe: Umwana akwimba lunofu.**
**N T E**

**Kiyao: Mwanache akwimba ucheneche.**
**N T E**

6. Fafanua mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia.

   a) **Zana lazima iendane na umri wa walegwa,**
   b) **iendane na mada ya somo husika,**
   c) **izingatie ukubwa wa darasa,**
   d) **ionekane vizuri na kuvutia,**
   e) **iendane na mada husika na muhtasari wa somo.**

7. Kwa kutumia hoja nne, fafanua kwa ufupi umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu wa kusoma kwa wanafunzi wa kidato cha I- IV.

   a. **kusaidia kutambua maandishi na maana iliyomo**
   b. **kukuza kasi na wepesi katika kusoma,**
   c. **Hujenga moyo wa kupenda kusoma**
   d. **huimarisha uwezo wa kugundua, Kuchagua na kupanga mawazo muhimu yaliyopo katika Habari iliyosomwa.**
   e. **Huimarisha kiwango cha matumizi yake ya lugha**

8. Chambua kwa ufupi mambo manne yanayoweza kufanywa na mwalimu katika hatua ya utangulizi wa somo anapofundisha mada ndogo ya *Aina za Maneno* (Nomino).

   a. **kujenga utayari wa wanafunzi**
   b. **kuwapa wanafunzi chemsha bongo/bungua bongo kuwauliza maswali mafupimafupi yanayohusu nomino,**
   c. **kuuliza maswali ya mada iliyopita,**
   d. **kuuliza maswali mepesi yanayochokonoa somo jipya**

9. Soma mfano wa hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Makamu wa Rais kisha jibu maswali katika vipengele vifuatavyo:

(a) Taja aina ya hotuba;
**Hotuba ya kiserikali**

(b) Toa sababu tatu za jibu katika kipengele (a).
**Inatolewa na kiongozi wa kiserikali ambaye ni Makamu wa Rais, ilitoa taarifa kuhusu kiongozi wa kiserikali na ilihusu shughuli ya kiserikali.**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA MAKAMU WA RAIS**

*Ndugu wananchi, wageni waalikwa, na viongozi wote mliohudhuria leo, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa kujitokeza kwa wingi katika shughuli hii muhimu ya kitaifa. Serikali yetu imeendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi wetu. Leo, tunazindua rasmi mradi wa maji safi na salama ambao utawanufaisha wakazi wa wilaya hii na maeneo jirani. Hili ni hatua kubwa katika kuhakikisha huduma muhimu zinawafikia wananchi wote kwa wakati.*

*Ndugu wananchi, serikali itaendelea kusimamia haki, usawa, na maendeleo kwa manufaa ya watu wote bila kubagua. Ninawasihi tushirikiane kwa upendo na mshikamano katika kutunza miundombinu hii ili idumu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Aidha, napenda kuwahakikishia kuwa serikali ipo tayari kusikiliza na kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi kwa wakati. Asanteni sana kwa kunisikiliza.*

10. Eleza kwa ufupi aina nne za upimaji atakazotumia ili kujua maendeleo ya wanafunzi wake kitaaluma.
   a) **upimaji wa awali ambao hufanyika kabla ya kuanza masomo au mada fulani,**
   b) **upimaji gunduzi ambao mwalimu huufanya anapokuta mwanafunzi wake ana tatizo Fulani katika kujifunza,**
   c) **upimaji endelezi ambao hufanywa wakati wowote kadri mwalimu anavyoendelea kufundisha mada zake**
   d) **upimaji tamati ambao unaofanywa mwishoni mwa mafunzo fulani**

## SECTION B (60 Marks)

Jibu maswali yote kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama **kumi na tano (15)**

**11. Thibitisha kwa kutumia hoja tano kuwa mhakiki ana mchango mkubwa katika uchambuzi wa kazi za kifasihi.**

Mhakiki ana mchango muhimu kwa sababu huchambua na kuweka wazi funzo linalotolewa na kazi ya fasihi. Katika kazi yoyote ya kifasihi, huwa kuna ujumbe au maadili yanayolengwa kufikishwa kwa jamii, na jukumu la mhakiki ni kulichambua funzo hilo kwa kina na kulielezea kwa njia ambayo wasomaji na watazamaji wa kazi hiyo wataweza kulielewa kwa urahisi.

Mhakiki pia huchambua na kufafanua picha za kisanii zilizotumika katika kazi ya fasihi. Kazi nyingi za kifasihi hutumia taswira, sitiari, tashbihi na mbinu nyingine za kifasihi kuwasilisha ujumbe wake. Kwa kupitia mchango wa mhakiki, msomaji anapata kuelewa maana ya picha hizo na namna zinavyosaidia kuimarisha kazi ya fasihi.

Jukumu lingine muhimu la mhakiki ni kumshauri mwandishi ili afanye kazi bora zaidi. Baada ya kuchambua kazi ya fasihi, mhakiki huweza kubaini udhaifu na uimara wake. Kupitia tathmini hiyo, mhakiki humpa mwandishi mapendekezo ya maeneo yanayohitaji kuboreshwa na jinsi ya kuongeza ubunifu katika kazi zake za baadaye.

Mhakiki humwelekeza msomaji ili apate faida zaidi kuliko yale ambayo angeweza kuyapata bila dira ya mhakiki. Mhakiki huweza kufafanua maana fiche au ujumbe uliositirika katika kazi ya fasihi, hivyo kumsaidia msomaji au mtazamaji kupata maarifa mapana zaidi kuliko yale angetambua kwa kusoma au kutazama peke yake.

Aidha, mhakiki husema ukweli ipasavyo kuhusu tamaduni na falsafa zinazotawala fasihi. Baada ya kuichambua kazi ya kifasihi, mhakiki hufafanua namna kazi hiyo inavyoakisi mila, desturi, na falsafa za jamii husika, hivyo kutoa mwanga kuhusu maisha ya jamii inayohusika na mabadiliko yake.

**12. Fafanua miundo sita ambayo kikundi nomino kinaweza kujidhihirisha na toa mifano miwili kwa kila muundo.**

Muundo wa umbo kapa (Ɵ) ni muundo wa kikundi nomino ambao hautamkwi katika mazungumzo lakini upo katika muundo wa ndani. Kwa mfano: *Hukumwona Subira?* ambapo 'wewe' haijasemwa wazi, na *Vilivyopotea vimepatikana?* ambapo 'vitu' havijasemwa moja kwa moja.

Nomino pekee ni pale ambapo kikundi nomino kina nomino peke yake bila kirai chochote. Mfano: *Meli imewasili ufuoni.* na *Ng'ombe ameingia shambani.*

Kiwakilishi pekee ni muundo ambapo kikundi nomino kinaundwa na kiwakilishi bila nomino. Mfano: *Wao wataondoka kesho.* na *Hili linanifurahisha.*

Nomino na Kivumishi ni muundo ambapo nomino inaambatana na kivumishi kinachoielezea. Mfano: *Wakulima hodari walivuna mazao mengi.* na *Wanafunzi wengi walifaulu mitihani.*

Kiwakilishi na Kivumishi ni muundo wa kikundi nomino ambapo kiwakilishi hufuatiwa na kivumishi kinachokielezea. Mfano: *Vile vyote vililetwa jana.* na *Zile chache zibaki.*

Nomino na Kirai Kivumishi ni pale nomino inapofuatiwa na kirai kivumishi kinachoielezea. Mfano: *Ng'ombe huyu wangu ni mweusi.* na *Magunia yenye sukari yalipakiwa humo.*

**13. Elezea misingi mitano utakayozingatia wakati wa utunzi wa maswali ya majibu mafupi.**
Katika kutunga maswali ya majibu mafupi, ni muhimu kuhakikisha swali linakuwa la wazi na lenye majibu ya moja kwa moja. Hii inamwezesha mwanafunzi kujieleza kwa ufasaha na kwa uhakika bila kuchanganyikiwa.

Ni lazima kuepuka kuchukua sentensi moja kwa moja kutoka kwenye kitabu cha kiada kama ilivyo, bali kutunga swali linaloendana na mada na kueleweka kwa mwanafunzi. Hii husaidia kupima uelewa halisi wa mwanafunzi badala ya kukariri.

Maswali yanapaswa kutungwa kwa lugha rahisi na inayoeleweka kwa urahisi kwa wanafunzi wa kiwango husika. Lugha tata au yenye muktadha mgumu huweza kuwachanganya wanafunzi na kushusha ufanisi wa tathmini.

Ni muhimu kuhakikisha swali linaendana moja kwa moja na malengo ya somo au kipengele kilichofundishwa. Hii inasaidia kupima kama mwanafunzi amefikia malengo ya somo hilo.

Mwisho, ni muhimu kuhakikisha maswali haya yanaweka mazingira ya kumpa mwanafunzi fursa ya kueleza mawazo yake mwenyewe kwa kifupi lakini kwa usahihi, bila kutumia sentensi ndefu au maelezo marefu yasiyo ya lazima.

**14. Fafanua namna ya kutumia kadi za maneno kufundishia aina za maneno katika hatua ya maarifa mapya na kukazia maarifa kwa kuonesha vitendo vya ujifunzaji na ufundishaji kwa kila hatua.**
Katika hatua ya maarifa mapya, mwalimu ataongoza wanafunzi kuchagua kadi za maneno ambazo zimechanganywa mezani. Wanafunzi watachagua kadi yenye aina ya neno lililolengwa, kwa mfano nomino, na kisha kutaja aina hiyo na kutoa mifano mingine.

Katika hatua ya kukazia maarifa mapya, mwalimu atatumia kadi kuongoza shughuli ya kutofautisha aina mbalimbali za maneno. Wanafunzi watachagua kadi zinazowakilisha aina tofauti za maneno kama vivumishi, vitenzi, viwakilishi na nomino na kueleza tofauti kati ya kila aina.

Vitendo vya ujifunzaji katika hatua ya maarifa mapya vitakuwa ni kuchagua na kutaja aina ya neno, huku mwalimu akielekeza na kurekebisha makosa. Katika kukazia maarifa, vitendo vitakuwa kutofautisha aina ya maneno na kutoa mifano sahihi ya matumizi yake katika sentensi.

Hii njia hujenga uwezo wa mwanafunzi kutambua, kutofautisha na kutumia aina mbalimbali za maneno kwa ufanisi ndani ya sentensi na maandishi, hivyo kumwezesha kuboresha lugha na ufasaha wake katika kujieleza.